



Ministère de l'Enseignement Primaire,
Secondaire et Professionnel

KUSOMA NA KUANDIKA

Kitabu ca mwanafunzi

KISWAHILI

3



Edition 2018



KUSOMA NA KUANDIKA

Kitabu ca mwanafunzi



Direction des Programmes Scolaires et Matériel Didactique

YALIYOMO

DIBAJI	1
INGILIO	2

KIPINDI CA 1 : KUISHI VIZURI NAFASI YAKO

Juma ya 1 : Kijiji	4
Juma ya 2 : Mji	8
Juma ya 3 : Ndoa	12
Juma ya 4 : Sherehe ya ceti	16
Juma ya 5 : Usafi wa mwili - usafi wa nguo na cumba	20
Juma ya 6 : Matunzo - Vituo vya afya	24

KIPINDI CA 2 : KUKINGA MAZINGIRA

Juma ya 8 : Mapishi	30
Juma ya 9 : Vinywaji	34
Juma ya 10 : Mimea - Mavuno	38
Juma ya 11 : Kukinga mazingira	42
Juma ya 12 : Nyama za ufugo	46
Juma ya 13 : Nyama za pori	50

KIPINDI CA 3 : KUENDELESHA JIMBO MBELE

Juma ya 15 : Kazi ya shamba	56
Juma ya 16 : Kazi ya mikono	60
Juma ya 17 : Barabara - wanda - maji	64
Juma ya 18 : Vyombo vya usafiri	68
Juma ya 19 : Micezo za asili	72
Juma ya 20 : Micezo	76

DIBAJI

Kifungo cha mwisho ya kanuni ya tano ya sheria muhimmo ya mafunzo ya taifa, inchini ya Kidemokrasia ya Kongo, kinajulisha kwamba, maadibisho ya shule ina ukomo ya kuelimisha kimuhimu na kiusawa kila mtu kusudi ya kumfanya awe mwenye mafaa kwake ye ye mwenyewe, pia kumuingiza ndani ya shirika.

Kwa kufikia ukomo hii, yapashwa, kwa mwisho ya masomo ya msingi, mtoto mkongomani aelewe , kusoma, kuandika, kuhesabu, kusikiya na kusema kwa luga la kikingomani na kifaransa.

Kwa hivi, hadi leo tena, kuna mwanafunzi anaye maliza masomo ya msingi na angali bado na magumu kati ya usomi-mwandiko; uwezo aliopata katika majifunzo ya kusoma na kuandika haifike kwenye kiwango za kanuni ya kimataifa.

Tokeo hii, inahakikisha na mitiani mbalimbali ya taifa (TENAFEP) na ya kimataifa (EGRA). Kiwango ya chini ya mafanikio inayo rikodiwa katika elimu zingine za shule, inazingatiwa kuwa matukio mbovu, ya wanafunzi, kukosa ujuzi wa kusoma na kuandika.

Uwezo wa usomi-mwandiko, inabaki shurti inayoitajika kwa kuhakikisha majifunzo ya elimu zingine.

Kwa kutengeneza hali hii, Wizara ya mafundisho ya msingi, sekondari na kazi, ilikamata hatua muhimu inayo lengo la kuboresha hali ya mafunzo-majifunzo, hasa kwa kutosha usomi-mwandiko kuwa elimu ndogo, na kuiinua kwa ngazi ya elimu kubwa ya majifunzo.


Ndio sababu, wizara ya mafundisho ya msingi, sekondari na kazi, anashukuru mchango ya washirika wake kiufundi na kipesa, kumuunga mkono kwa uboreshaji wa hali ya majifunzo na kwa ubadili ya mfumo kielimu ya Kongomani.

Vitabu hivi, vimeundwa na chumba inchini, kinacho usika na mipango ya shule na vyombo vya mafunzo (DIPROMAD) ikisaidiwa na washirika wanao jiusisha na mafunzo ya usomi-mwandiko kwa luga la taifa. Vitabu hivi, ni mali ya Wizara ya mafundisho ya musingi, sekondari na kazi, pia ni kwa wanafunzi na walimu wa darasa la kwanza, la pili na la tatu ya shule zote ya msingi ya kiserkali na ya msingi ya kipekee yenye kukubaliwa. Tuna amini, watashiriki kwa uboreshaji wa mafundisho na majifunzo.

Walimu wanaume na wanawake, wanaitwa kwa kufanyiziya na kutumia kwa upeo vyombo hivyo vya bei vya mafundusho kwa kufanya kazi zao zaidi kwa faida ya wanafunzi

Gaston MUSEMENA BONGALA

*Waziri wa Mafundisho ya
Msingi, Sekondari na Mtaalamu*



INGILIO

Waziri wa Jamuhuri ya kidemokratia ya Kongo aneye husika na mafunzo ya msingi, sekondari na kikazi, anainua elimu ndogo ya kusoma na kuandika kwa kiwango ya elimu kubwa incini. Alikamata mpango huu, ili ajibu ku maendeleo ya kikanda na kimataifa, kulingana na kanuni zilizo cukuliwa duniani kote pamoja na yanayo fanyika inchini mwetu.

Kwa kuboresha hali ya mafunzo-majifunzo ya kusoma na kuandika kunako shule la msingi, uwaziri huo, umeandalia mwanafunzi na mwalimu vitabu kufuatana na mpango wa mafunzo ya taifa.

Kwa darasa ya kwanza na ya pili ya shule la msingi, luga ya taifa iko kwa ujumla, luga ya mafunzo na elimu inayo fundishwa. Kwa darasa izo mbili, kifaransa inafundishwa tu sawa elimu. Mafunzo yake, inaishia tu kwakusema bila kuandika.

Ni kuanzia kwa darasa ya tatu ndipo majifunzo kwa luga ya taifa yanahamishwa kwa luga la kifaransa. Ni wakati misingi ya ufundi wa kusoma luga la taifa limekwisha tiwa, ndipo, wanafunzi watajifunza sasa bila shida na kwa haraka luga la kifaransa.

Maendeo ya mafunzo-majifunzo inatiya msingi kwa kulinganisha luga la kwanza na lile la pili. Kwa hivyo, vikundi tatu vya herufi vilitambulishwa:

- Herufi za kufanana kwa sauti na kwa maandiko;
- Herufi za kufanana kwa maandiko lakini zina sauti mbalimbali;
- Herufi za kipekee.

Buku la usomi la mwanafunzi, pamoja na kitabu cha mwalimu na cha mwanafunzi, viliundwa kwa misingi wa ugunduzi wa kisayansi ya sasa, inayo hakikishwa na kucunguzwa.

Ndani ya maendeleo ya mafunzo-majifunzo, msingi ni juma ya majifunzo. Kila juma ya mafunzo-majifunzo, ina mada ndogo inayo fundishwa katika siku sita ya kifaransa na siku ine ya luga la taifa. Siku ya kwanza ya juma, wanafunzi wanasikiliza usomi wa mwalimu. Siku ya mwisho, wanafunzi wanakamilisha yale waliojifunza juma nzima, na wanafanya mazoezo ya kuandika.

Kitabu hiki, ni chombo nzuri kiliotungwa kwa kuimarisha mazoezo mbalimbali yalio fanyika somoni. Tunaalika walimu pia wazazi kusindikiza wanafunzi na kuwapa nguvu ya kumiliki yalio ndani ya kitabu hiki Tajiri kwa mazoezo ya kusoma na kuandika, ambao, bila shaka kitawaruhusu kupata ujuzi unayo hitajika.


KIPINDI CA KWANZA

KUISHI VIZURI NAFASI YAKO

Mazingira

Kijiji

Nazungumuza hadisi hii.



Natazama.



Nasoma.

Mapendo ya Kijiji

Paulo ana mapendo ya Kijiji cake. Kila mara anawaza nini atafanya. Asubuhi, Paulo alikusanya vijana wote akawaambia: «Sisi ndiyo viongozi vyat wakati ujao».

Tukamate mipango ili tutie usafi kijijini. Wamoja watafyagia barabara kila siku. Wengine watakata majani mabaya. Watoto nao watatupa ucafu ndani ya yalala. Wote wanatumika ili waepuke mbu.

Naandika ile nitafanya kwa kuonyesha mapendo ya kijiji cangu.

Nacagua ndani ya usomi, misemwa mbili ya kuhakikisha.

1.



2.

Naandika ingine misemwa ya kuhakikisha.

1.

2.

Naandika jina ya sanamu ndani ya buku ya mazoezo.



A horizontal line consisting of 20 small black circular dots arranged in a single row.

.....

.....

Najaza msemwa huu:

Katika Kijiji cetu muna

Naeleza kwa kuandika misemwa mbili ya hali ya Kijiji cetu.

Mazingira

Mji

Nazungumuza hadisi hii.



Natazama.



Nasoma.


Matembezi katika mji

Paulo na wenzake wanaenda matembezi katika mji.
Wanaona duka mingi inawashangaza.

Gari na pikipiki zinapita mbio sana. Wanaogopa kuvuka
barabara. Wakajiuliza: “Tufanye je ili tuvuke njia?”
Wakashikana mikono.

Wanaona pia serkali kubwa ya mji wetu. Wanafurahi
jinsi nyumba za gorofa zimejengwa.

Naandika ile nitafanya wakati naenda matembezi
katika mji wangu.



Nacagua ndani ya usomi, misemwa ya kuuliza kiisha uiandike.

1.



2.

Naandika ingine misemwa mbili ya Kuuliza.

1.

2.


Naandika jina ya sanamu ndani ya buku ya mazoezo.



Najaza msemwa huu:

Wapi kila posho?

**Naeleza kwa kuandika misemwa mbili, fasi wazazi
wanaenda kila posho.**



Sherehe

Ndoa

Nazungumuza hadisi hii.



Natazama.



Nasoma.


Tumealikwa ku karamu

Sisi tumealikwa ku karamu ya ndoa. Tunatayarisha mavazi yetu vizuri. Tunafika ku karamu tunapeleka zawadi yetu.

Baadae, tunakula cakula na kunywa vinywaji mbalimbali. Mimi nafurahi kabisa na matunda.

Wakati tunamaliza kula, tunaceza malinga ya kwetu. Nkambo hakuceza sababu ni mgonjwa. Bibi na bwana arusi wanaceza vizuri sana sababu ni siku kuu yao.

Naandika kitu nitakaefanya wakati wa ndoa ya ndugu wangu.



Natia misemwa hii kwa sura ya kukana.

1. Sisi tumealikwa ku karamu.

.....

2. Nilipeleka zawadi nzuri.

.....

Naandika misemwa mbili ya kukana.

1.

2.

Nacagua neno isiyo angalia ndoa.

Arusi

Mtumbwi

Cakula

Bwana

Nyimbo

Najaza msemwa huu:

Ku ndoa tunahitaji

Naeleza kwa misemwa vitu mbalimbali ninavyohitaji ku karamu ya ndoa.

Sherehe

Sherehe ya ceti

Nazungumuza hadisi hii.



Natazama.



Nasoma.

Kiisha karamu

Karamu ilipita vizuri sana, cakula ilikua mingi. Tunakula, kunywa na kuceza malinga.

Wajumbe wa masomo wanafurahi pia. Mbele warudi wanamtolea Nehema msaada.

Sisi tunaendelea kuceza mpaka mangaribi. Kiisha tunasafisha masahani yote. Tunahesabia msaada na zawadi. Maua ni mingi. Amisi hakutumika tena analala.

Naandika kitu nitakaefanya wakati wa karamu.

Najaza vyumba.

Nafsi	Nyama	Vitu

Naandika misemwa tatu: moja na jina la mtu, na jina la nyama na la mwisho na jina la kitu:

1.
2.
3.

Nacagua neno isiyo angalia Karamu.

Vazi

Vigelegele

Furaha


Ceko

Fimbo

Najaza msemwa huu:

ku karamu tunahitaji.....


Naeleza kwa misemwa vitu mbalimbali ninavyofanya
ku karamu.



Afya

Usafi wa mwili, nguo na cumba

Nazungumuza hadisi hii.



Natazama.



Nasoma.

Mafundisho ya mganga

Alina anafasiria wazazi somo ya mganga. Mganga alifika somoni. Alitupatia mashauri ya usafi.

Mganga alitufundisha ginsi tunaweza kuepuka magonjwa. Tukisukua meno na muswagi na kugoma mavazi.

Tukibadilisha nguo ya kitanda kila mara. Tukifungua madirisha ya cumba yetu.

Naandika maneno inayo elekea usafi wa mwili.

A large rectangular grid divided into a 10x15 grid pattern, designed for children to practice their handwriting skills by writing the Swahili sentence provided above it.

Naandika majina tatu ndani ya kila cumba.

Jina la pekee	Jina la jamii

Naandika misemwa tatu: moja na jina la mtu, mwengine jina la nyama na la mwisho na jina la kitu.

1.
2.
3.

Naandika maneno tano inayoelekea usafi.

Najaza msemwa huu:

Tufue nguo ili
.....


Naeleza kwa kuandika misemwa mbili ya vitendo vya usafi.

A large rectangular grid of squares, likely a worksheet for drawing or writing practice. The grid consists of approximately 20 columns and 10 rows of small squares.

Afya

Matunzo - vyumba vya afya

Nazungumuza hadisi hii.



Natazama.



Nasoma.


Waganga wenyi ujuzi

Hopitali ya kijiji cetu ina waganga wengi. Wana ujuzi kabisa. Wanatunza magonjwa mbalimbali.

Kila mganga anakazi yake ku hospitali. Ukiwatafuta waganga wa: meno, moyo, maco utawapata pia kuna waganga wa watoto.

Hata kama umevunjika mguu, utapata mganga. Sisi tuende hospitalini wakati tunagonjwa, kiisha tufwate mashauri ya waganga.

Naandika maneno mbalimbali inayo elekea vituo vya afya.



Najaza kadi hii na majina ku uwingi ao ku umoja.

Nafsi	Nyama	Vitu
Safi	Imbwa	cakula



KIPINDI CA PILI

KUKINGA MAZINGIRA

Cakula

Mapishi

Nazungumuza hadisi hii.



Natazama.



Nasoma.

Cakula kawaida

Nyuma ya nyumba yetu, kuna bustani. Chiza alicuma majani ya viazi ya bustani. Majani ya viazi ni mboga kawaida. Inakinga mwili wetu kwa matatizo ya afya.



Chiza anapiga majani ya viazi. Anaongeza viungo: tomati, matunguu na kazalika. Wakati inaivia Chiza anaonja, anaruka ruka na furaha. Anasema: «Huum! Mcuzi huu ni tamu sana!»

Naandika majina mbalimbali ya cakula.

Naandika majina hii kwa uwingi ao umoja.

Umoja	Uwingi
Kinywaji	
	Viazi
Kiungo	
	vitabu
Kiti	
Kidole	

Naandika jina ya sanamu ndani ya buku ya mazoezo.



• • • • • • • • • • • • • •

• • • • • • • • • • • • • •

• • • • • • • • • • • • • • •

Najaza msemwa huu:

Nyumbani tunakula

Naeleza kwa kuandika misemwa mbili ya vyakula kawaida ninavyopenda.

A large rectangular grid consisting of 10 columns and 10 rows of small squares, designed for drawing or writing practice.

Cakula

Vinywaji

Nazungumuza hadisi hii.



Natazama.



Nasoma.

Kisima ca kijiji cetu

Kijiji cetu kina kisima ya maji safi. Kila mwanakijiji anatega maji ku kisima. Tunafanya angalisho wakati tunatega maji. Sababu ni maji ya kunywa, hatupendi ucaf uingie ndani.



Kwa kuinga usafi wa kisima, kila jamaa ina posho moja ya kutia usafi. Kweli maji ya kisima cetu ni bora.

Naandika maneno mbalimbali inayo elekea vinywaji.

Naandika majina hii kwa uwingi ao umoja.

Umoja	Uwingi
Muanakijiji	
	Wanaume
muke	
	Watoto
mutu	

Naandika jina ya sanamu ndani ya buku ya mazoezo.



.....

.....

.....

Najaza msemwa huu:

Kila asubuhi tunakunywa

Naeleza kwa kuandika misemwa mbili ya vinywaji
ninayotumia baadae kula.

A large rectangular grid divided into a 10x10 pattern of smaller squares, designed for handwriting practice.

Pori

Mimea - Mavuno

Nazungumuza hadisi hii.



Natazama.



Nasoma.

Mafaa ya pori

Leila na Davido wanaenda kulunguza pori. Wanabeba kibiriti. Ni wakati wa kipwa. Njia ni nyembamba na miti ni mirefu. Matawi ni mengi na na yenzi kukauka. Wanasikia mlio mzuri wa ndege, wa wanyama na vidudu vya kila aina.

Davido akasema: «Tukiunguza pori, miti itaungua na wandege watifariki.»

Leila anasema: «Pori yatupatia cakula. Wanyama ni mali ya inci yetu.»

Na hivi, wanarudi kwao.

Naandika maneno mbalimbali inayo elekea mimea.

A large, empty rectangular grid divided into a 20x10 grid pattern, enclosed within a thin black border. This grid is intended for children to practice writing the Swahili words from the story.

Naandika majina hii kwa uwingi ao umoja.

Umoja	Uwingi
Mhogo	
	Miguu
Mhindi	
	Miti
Mlima	

Nacagua neno isiyo angalia mimea na mavuno.

Maboga

Kupanda

Avokati

Samaki

Maharagi

Najaza msemwa huu.

Kwa kukinga mazingira, tunapashwa

Naeleza kwa kuandika misemwa mbili namna nitatumia mavuno.

Pori

Kukinga mazingira

Nazungumuza hadisi hii.



Natazama.




Nasoma.

Tuheshimu mto

Mto ni yenyi mafaa kwetu. Inasaidia watu, nyama pia mimea. Watu wanaishi kandokando ya mto. Wanajiosha na kuivisha cakula kwa maji yake.

Kucafua mto imekatazwa. Tukumbuke watu wanaoishi cini ya mto. Samaki pia wanahitaji maji safi.

Naandika maneno mbalimbali inayo elekea kukinga mazingira.



Tokea usomi, nacagua maneno 4 inayo onyesha mwenyeji wa tendo.

Naandika msemwa ambao mwenyi wa tendo ni jina.

Nacagua neno isiyo angalia Pori.

Miti

Buku

Jito


Majani

Nyama

Najaza msemwa huu.

Pori inatusaidia kwa

Naeleza kwa kuandika misemwa mbili vitendo
ninavyojuu vyatukinga mazingira.




Nyama

Nyama za ufugo

Nazungumuza hadisi hii.



Natazama.




Nasoma.

Paka yetu

Nyumbani tunaishi na paka pembeni, jina lake Tomi. Mama na baba wamemubeba kila jioni. Wakati alikuwa mdogo, tulimulisha kwa maziwa.

Leo amewinda panya mwenyewe. Tomi hapendi maji lakini ni msafi. Amejiosha na ulimi wake. Nyumbani, tunamupenda Tomi sisi wote.

Naandika majina mbalimbali ya nyama za ufugo.



Tokea usomi, nacagua misemwa mbili: moja unayo timizo la karibu, mwingine na timizo la mbali.

1.....

2.....

Natunga misemwa mbili, moja unayo timizo la karibu, mwengine na timizo la mbali.

1.....

2.....

Naandika maneno 5 inayoelekea nyama za mji.

Najaza msemwa huu:


Nyama wamejilisha kwa

Naeleza kwa kuandika misemwa mbili, kazi mbalimbali ya paka nyumbani.

Nyama

Nyama za pori

Nazungumuza hadisi hii.



Natazama.




Nasoma.

Mamba na Kima

Mamba anaomba kima wawe marafiki. Tutaishi namna gani ? Ulizo la kima kwa mamba. Mimi nakaa mitini, nimejilisha kwa mbegu. Ila wewe umelala majini, na umejilisha kwa samaki.

Mamba akasema: «tutaishi mcana, nakuacana usiku.» Vema, inawezekana tuwe marafiki, kwakuwa tunaishi porini. Mamba na kima wakawa marafiki wazuri.

Naandika maneno mbalimbali inayo elekea nyama za pori.



Ndani ya usomi yetu, cagua misemwa mbili: moja unayotimizo la mahali, mwingine na timizo la wakati.

1.....

2.....

Natunga misemwa mbili, moja unayo timizo la mahali, mwingine unayotimizo la wakati.

1.....


2.....

Naandika maneno inayoelekea nyama za pori.

Najaza msemwa huu:

Nyama wamejilisha kwa

Naeleza kwa kuandika misemwa mbili kitu ninaweza kufanyia mtu akiniomba msaada.

A large rectangular grid consisting of 10 columns and 10 rows of small squares, designed for drawing or writing practice.




KIPINDI CA TATU

KUENDELESHA JIMBO MBELE

Kazi

Kazi ya shamba

Nazungumuza hadisi hii.



Natazama.



Nasoma.

Mavuno

Mashauri ya baba inasaidia watoto. Wakati wa mavuno wanajaza tele mifuko ya cakula. Mavuno hio ndiyo utajiri baba yao aliwaambia.

Kusudi isioze, wanaweka maharagi ndani ya mifuko.
Wanapanga mihogo kwenye jua ili ikauke vizuri. Matunda
na mamboga wanaziweka pa nafasi nzuri. Kwa furaha,
wanaeupuka kabisa njaa mwaka huu.

Naandika maneno mbalimbali inayo elekea kazi ya shamba.

Ndani ya usomi yetu, nacagua vielezo 3 ninavyo tambua.

1.....

2.....

3.....



Natunga sasa msemwa na kila kielezo niliyocagua.

1.....

2.....

3.....

Naandika jina ya sanamu ndani ya buku ya mazoezo.



.....


.....

.....

Najaza msemwa huu:

Tunapandatele.



Naeleza kwa kuandika misemwa mbili namna
ninalima shamba.




Ufundi

Kazi ya mikono

Nazungumuza hadisi hii.



Natazama.




Nasoma.

Mama ni mshonaji

Mama ameniamsha kila asubuhi nifyagie nafasi ya kushonea. Ninapo maliza ameniomba pia meza na viti.

« Nitashona leo nguo nydingi! » Asema mama. Wateja wangu wanahitaji kesho nguo zao. Ninapokata nguo, musiokote ovyo vitepe. Kuna vitepe nitakavyo tumikisha upya. Mtu asishike mkasi na wembe mezani mwangu.

Naandika maneno mbalimbali inayo elekea kazi ya mikono.




Ndani ya usomi yetu, nacagua kielezo ya kulinganisha,
ya kiasi, ya wakati na ya mahali.

1.....
2.....
3.....
4.....

Natunga sasa msemwa na kila kielezo niliocagua.

1.....
2.....
3.....
4.....

Naandika jina cini ya sanamu.



.....

.....

.....

Najaza msemwa huu:

Baba amerudi kila na pesa nyumbani





Naeleza kwa kuandika misemwa mbili ya kazi
mbalimbali ya mikono ninayofurahia.

A large rectangular grid divided into 24 equal squares, intended for the student to write the sentence provided above it.

Usafiri

Barabara - wanda - maji

Nazungumuza hadisi hii.



Natazama.



Nasoma.

Mto Kongo

Mto Kongo ni mrefu na mnene. Ni mto unayo katiliza Kongo-Kinshasa nzima. Watu wanaweza kusafiri kwa maji yake.

Tumieni mtumbwi ao mashua kwa kusafiri. Wengine waloe samaki. Maji yake ni nzuri na yenye umeme ngumu. Jito Kongo inajaa kwa mvua pia kwa vijito.

Naandika maneno inayo elekea njia ya usafiri.

A large rectangular grid consisting of 10 columns and 15 rows of smaller squares, designed for children to practice writing letters and words.

Ndani ya usomi yetu, nacagua maelezo 3 la hali ninayo tambua.

1.....

2.....

3.....

Natunga sasa msemwa na kila elezo la hali niliyocagua.

1.....

2.....

3.....

Natafuta neno isiyo angalia njia.

Barabara

Jito

Kitanda


Bahari

mashua

Najaza msemwa huu:

Barabara yetu ni


Naeleza kwa kuandika misemwa mbili njia
mbalimbali ya usafiri ninayo zoea.



Usafiri

Vyombo vyatofauti

Nazungumuza hadisi hii.



Natazama.




Nasoma.

Kinga ya mjomba

Mjomba amepokea kinga nyeusi mpya. Vyumba vyake vya hewa ni vyeusi pia. Jioni mjomba anacunguza hewa ndani ya gurudumu.

Kesho nitaenda shambani kubeba mavuno. Njia ina bonde ndefu pia milima mbili mirefu. Mapema nitaweka breki na kibeba-mizigo. Nitahitaji pia kamba kwa kufunga mizigo.

Naandika maneno mbalimbali inayo elekea vyombo vya usafiri.



Naandika kwa uwingi ndani ya buku ya mazoeo:

Umoja	Uwingi
Cumba ceusi
Mlima murefu
Mutu mupumbavu
Bonde mufupi

Natunga msemwa na kila elezo la sura lifuatayo:
mpya, mapya, mdogo.

2.
2.
3.

Naandika maneno inayoelekea vyombo vya usafiri.

.....

.....

.....

.....

Najaza msemwa huu:

Kwa kusafiri tunahitaji

Naeleza kwa kuandika, misemwa tatu vyombo gani ninacukua kwa kusafiri.

Micezo

Micezo za asili

Nazungumuza hadisi hii.



Natazama.




Nasoma.

Kutayarisha mcezo

Tunatayarisha mcezo ya kukimbia. Kama sijitayarische vizuri, siwezi kushinda. Siwezi kushinda sababu, wapingaji wangu wanajitayarisha vizuri.

Navaa vazi inayofaa ili ngozi ya mwili ipate hewa. Kama jua ni kali, navaa kofia kicwani. Kofia yanisaidia kwa kuepuka joto. Sasa niko tayari. Siogope hatu kitu sababu niko tayari kwa kuceza.

Naandika maneno mbalimbali inaelekea micezo za asili.



Naandika matendo wa wakati utakaokuja.

Wakati wa sasa	Wakati utakuja
Ninatayarisha	
Anaceza	
Tunawina	
Tunavaa	

Naandika matendo wa wakati wa sasa.


Wakati utakaokuja	Wakati wa sasa
Nitakula	
Atakuja	
Tutakimbiya	
Wataogopa	

Naandika maneno inayoelekea micezo ya asili.

Najaza msemwa huu:

Mbele ya kuceza tuna.....


Eleza kwa misemwa tatu matayarisho gani ninafanya
kwa kushinda mcezo.



Micezo

Micezo

Nazungumuza hadisi hii.



Natazama.



Nasoma.

Mcezo inaanza

Mcezo wa kukimbia unaanza. Tino na Tina ni wahuzuriaji. Wanatazama ginsi mcezo inapitika.

Wacezaji wanakimbia mbio sawa vile kasha. Gola ana mbio sana lakini anateuka. Hakuweza kufika wa kwanza. Tino na Tina wanapiga mikono na kuimba nyimbo.

Tina analalamika wakati timu yake inakimbia. Tino yeye anafurahi ginsi wacezaji wanakimbia.

Naandika maneno mbalimbali inayo elekea micezo.

A large rectangular grid divided into a 10x15 grid pattern, designed for children to practice writing letters or words in Swahili.

Nacagua ndani ya usomi, tendo tatu inayo anza na
kitangulizi « Ku ».

1.....

2.....

3.....

Naandika msemwa moja na kila tendo.

1.....

2.....

3.....

Naandika maneno inayoelekea micezo wa mpira.

Najaza msemwa huu:

Kwa kuceza mpira nina

Eleza kwa misemwa tatu namna munafanya kwa kujaza
mpira.

Ce manuel de l'élève a été imprimé grâce à l'appui généreux du peuple américain et du peuple britannique, à travers l'Agence des Etats-Unis pour le Développement International (USAID) et le Ministère Britannique de la Coopération Internationale (DFID/UKAID).



USAID
FROM THE AMERICAN PEOPLE

